kuliongoza taifa hili, wajifundishe lugha hii. Ni lazima ujue ya kwamba kukosa kwako kuzungumza na kuielewa lugha ya Kiswahili vizuri ni pigo kubwa sana kwako kama unataka kuongoza. Ni lazima tukubali kuwa lugha ya Kiswahili huunganisha wananchi wengi sana katika taifa letu. Kwa hivyo, kiongozi yeyote ambaye ana nia ya kutaka uongozi wa taifa hili ni lazima afahamu lugha ya Kiswahili kikamilifu kwa kuizungumza, ili aweze kutoa maoni yake juu ya mabadiliko ya Katiba kwa lugha hii.

Bw. Naibu Spika, vyyo vyetu vya kitaifa vinasomesha lugha ya Kiswahili, lakini vinasomesha kama lugha ya pili. Wanafunzi wanaochukua lugha hii kama somo ambalo wanataka kupata shahada, huwa na shida nyingi. Utaona kima kinachopewa lugha hii ni hafifu sana kikilinganishwa na kima kinachopewa wanafunzi wanaosoma lugha za Kiingereza, Kifaransa na kadhalika. Jambo hili halimaanishi kuwa wasomi na wahadhiri katika vyyo vikuu hawana uhodari wa kusomesha lugha hii, hakika kuna upungufu wa vifaa, vitabu na njia za kufanya utafiti juu ya lugha hii. Mambo haya ya utafiti wa lugha, isipokuwa zile za kigeni, hayatiliwi maanani sana. Hapa nchini tunajishughulisha sana na lugha ya Kiingereza kwa sababu ndio lugha tuliorithi kutoka wakati wa zama za ukoloni. Leo, kama nilivyosema, kisaikolojia utaona ya kwamba mtu anaona yeye ni hodari zaidi na bingwa kumshinda mwingine kwa sababu anaweza kuzungumza Kiingereza zaidi kuliko lugha ya Kiswahili kwa sababu ni urithi alioupata kutoka kwa wakoloni. Fikira hiyo inamfanya kuona kuwa lugha ya Kiswahili ikifanyiwa utafiti ni kupoteza wakati na kuharibu rasilimali za taifa na kadhalika. Lakini kama alivyosema mhe. Kathangu, lugha moja ya kitaifa ambayo tutakubaliana imejitokeza kama lugha ambayo ni rahisi kuifahamu na kuikuza, na ambayo hutuunganisha katika tamaduni zetu, uzalendo, umoja, utetezi wetu na kadhalika ni lugha ya Kiswahili. Ni lazima tuitilie nguvu na kuikuza kikamilifu. Ikiwa sisi tumekomaa kiumri na kuwa wapevu zaidi, na kuona wakati wetu wa kujifundisha lugha ya Kiswahili umekwisha, tuisahau kuwa sisi si watu wa mwisho katika dunia hii. Tuna haja ya kujiunganisha katika taifa letu na kujiunga na wenzetu ambao wanazungumza lugha ya Kiswahili ulimwenguni. Leo lugha hii inazungumzwa kule Afrika ya Kati, Afrika ya Kusini, Uarabuni, Marekani, Canada na nchi nyingine nyingi. Kwa sababu hiyo, kubaki nyuma kwetu kwa lugha ya Kiswahili katika taifa letu na katika Afrika Mashariki ndio leo iliyosababisha watu watawanyike katika pembe zote za dunia. Kiswahili kimetawanyika katika pembe zote za dunia.

Bw. Naibu Spika, kwa hivyo, ni lazima tuwe na fahari na hata tukuze na tukubali Kiswahili kama lugha moja rasmi katika dunia hii. Kwa nini Kiingereza, Kifaransa na lugha nyingine zote tu ndizo zinazotambulikana? Saa nyingine, tunafikiri kwamba Kiswahili hakijitoshelezi, lakini tunaweza kuangalia isilahi ya neno la HIV/AIDS; Ukimwi. Hata neno lenyewe la Kiingereza halikuwa katika Kamusi ya Kiingereza. Mabingwa wa lugha, maradhi na sanyansi walikaa na wakaunganisha zile isilahi za neno lile na wakalitoa neno AIDS na hivyo ndivyo walivyofanya wabingwa wetu wa lugha ya Kiswahili na wakalitoa hili neno la Ukimwi.

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika, naunga mkono Hoja hii, kwani iko haja ya kuundwa kwa Baraza la Lugha za Taifa (BALUTA).

(Applause)

(Question proposed)

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, nashukuru kwa kunitunikia fursa hii nami nichangie kidogo angalau. Kama mbara wa kawaida, nalemewa na msamiati; siwezi kuongea Kiswahili maridadi kama mwenzetu, Bw. Badawy, kutoka Malindi. Ningependa kumshukuru rafiki na ndugu yangu, Mtumishi Kathangu, kwa kuleta Hoja ya maana Bungeni. Nafikiria tukiitumia vizuri, itakuwa ya maana kihistoria, na huu uwe mwanzo. Mfano huu uwe uzinduzi wa vuguvugu la kueneza Kiswahili katika Kenya.

Shida moja tulionayo katika hili Bunge ni kuwa wengi wa wale Wabunge ambao wanahitaji kuhamazishwa zaidi juu ya utenzi na utumishi wa Kiswahili wametoka nje wakati tunapoongea juu ya hilo jambo. Wale Wabunge ambao tungewaelezea juu ya shida wanazokabiliwa katika utumishi wao wa Kiswahili hawako hapa sasa. Wale wameona na wametambua maana ya lugha ya taifa na jinsi vile lugha inaweza kuchangia uzalendo wetu ndio wamebaki hapa, na ni wachache sana. Hilo ndilo jukumu letu, na sijui tutalieneza namna gani, hasa kwa wale wanaokaa zaidi sehemu hiyo karibu na mlango wa kuingilia Bunge hili. Unajua ni akina nani ninaongea juu yao. Nao pia wajihusishe na kujihamasisha kujifunza utenzi na utumizi wa Kiswahili.

Bw. Naibu Spika, kuna tofauti mbili kubwa sana zinazomhusu mgeni anapozuru Tanzania na Kenya. Kwanza, nitaongea juu ya mtalii. Mtalii anapoingia Tanzania, wenyeji humfundisha Kiswahili kidogo ili aanze kuwasalimu watu na kuuliza vitu vya kununua. Akija Kenya, tunafanya utoto. Tunamfundisha maneno machache ya kuimba tu, kama rekodi ambayo imeharibika: "Hakuna matata; iko matiti."

(Laughter)

Lakini hatuoni kama hiyo ni fursa ya kueneza heshima kwa lugha yetu, kwa sababu sisi wenyewe hatuheshimu Kiswahili chetu. Ukichukua mfano wa mwekezaji wa mitaji, kwanza kabisa anapoingia Tanzania, huenda katika taasisi fulani ili ajifunze Kiswahili, kwa sababu akiajiri watu kazi, atakuwa akiwaongelesha kwa Kiswahili. Akiita mtu, au aajiri mtu mwingine kutoka nje ya Tanzania, kwa sababu yeye ana mahitaji yake na fursa hiyo, huyu mtu naye itambidi ajifunze kuzungumza Kiswahili.

Bw. Naibu Spika, katika Kenya, Kiswahili ni lugha ya taifa, lakini mwekezaji akitoka nje na mitaji yake na awekeze Kenya, wewe Mkenya ni lazima uonyeshe ya kwamba unaweza kuongea Kiingereza ndio upate kazi. Kufuzu kwako na kutumia Kiswahili hakuna maana kwani huwezi kupata kazi katika nchi yako. Tunaendelea kujigamba ya kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya.

Bw. Naibu Spika, wengi wetu ambao tulizaliwa baada ya Mau Mau na tulioko hii leo, wengine wamekuwa na bahati ya kuwa na wazazi walioenda shule. Wakati huo, kuonyesha kwamba umesoma na umeerevuka kulikuwa ni kujitahidi sana kuongea Kiingereza. Watu wa makamu na wako hai sasa wamepitia huu muda ambao ulikuwa uonyeshe wewe umesoma kwa kuongea Kiingereza. Huku kukiwa na mahitaji ya kuwasiliana na wananchi wazalendo, inatubidi tujaribu Kiswahili. Matokeo yake yamekuwa nini---

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika. Vile nilivyomsikiliza mhe. Kituyi, nafikiri anapotosha hili Bunge kwa kusingizia ya kwamba Hoja hii inahusu Kiswahili. Vile nilivyosikia, Mtumishi Kathangu anataka kubuniwa kwa Baraza la Lugha za Taifa (BALUTA) ambazo ni lugha zaidi ya moja. Lakini Dr. Kituyi anaendelea kuweka mkazo lugha ya Kiswahili; ni kama anafikiria BALUTA itashughulikia lugha moja tu. Katika BALUTA, kusema ukweli iko kiswahili---

Dr. Kituyi: Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika---

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Bw. Kituyi, sijamaliza. Shika adabu na kaa chini. Katika BALUTA, iko Kiswahili, Kijaluo, Kikikuyu, Kiluyia na lugha nyingine. Hivyo ndivyo ninavyoelewa. Nataka aelewe hivyo na wakati nitakapochangia Hoja hii, ningetaka nifafanuliwe zaidi.

Mr. Deputy Speaker: Lakini Mtumishi Kathangu hajamaliza kuongea. Hatujui kama katika zamu ya pili ataingilia lugha za Kiluyia, Kiluo au Kikamba. Kwa hivyo, Hoja inaendelea.

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika---

(A mobile phone rang)

Mr. Deputy Speaker: Order, Dr. Kituyi!

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, sio mimi mwenye hiyo simu.

Mr. Deputy Speaker: Nani mwenye simu hiyo? Tafadhali, mwenye simu hiyo atoke nayo nje saa hii.

(Mr. Nderitu stood up in his place)

Mr. Deputy Speaker: Jitoe na hiyo simu yako kwanza!

(Mr. Nderitu withdrew from the Chamber)

Endelea, Dr. Kituyi.

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, ukifanya uchimbuzi wa Kinifu, utakumbuka kwamba mwenzangu hajafahamu zile mila zetu kuhusu kuchangia Mswada na Hoja katika Bunge. Anafikiria ya kwamba ni lazima katika kila sentensi niseme: "Lugha hii pia itumike kwa mawasiliano kwani ndiyo nzuri." Dr. Anangwe, nitakupa fursa ya kusema kwa nini tuongee Kiluhya katika Bunge. Nina haki kuongea juu ya lugha moja ya kitaifa, kama inaweza kuchangia kwa matumizi ya lugha za taifa. Kwa hivyo, niwache niongee juu ya Kiswahili. Ninasema nguzo za utu wetu kama Wakenya ni yale tutakayowaachia watoto wetu, na hii inatokana na vile tuna fikara endelevi, au vile tutaendelea kuonyesha ufukara wa mawazo.

(Laughter)

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika. Haja ya mzungumzaji yeyote ni kueleweka. Lakini mimi sielewi anachosema mhe. Kituyi.

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, tangu nichaguliwe katika hili Bunge sijaona kosa la kuelewa matumizi ya msamiati kuliko Wabunge wengine. Ikiwa mwenzangu amelemewa, inafaa atafute mbinu zinazoweza kumsaidia

kuutoa huu ufukara wa matumizi ya Kiswahili.

Mr. Deputy Speaker: Lakini inafaa wakuelewe!

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, mimi ninaelezea historia.

Mr. Deputy Speaker: Mhe. Kituyi, Mbunge akisimama kwa jambo la nidhamu, anaelekeza swali hilo kwa Bw. Spika na wala si kwa mzungumzaji.

Endelea!

Dr. Kituyi: Bw. Naibu Spika, ikiwa wewe ndio unaulizwa ubadilishe msamiati ninaoutumia kwa sababu mwenzangu hafahamu Kiswahili, ninafikiri itakuwa vigumu kwako kumsaidia. Inafaa umshauri arudi shuleni.

Bw. Naibu Spika, ningependa kuwauliza wenzangu: Huu mstakabali tunaotaka watoto wetu wastahimili, utakuwa mstakabali gani kwa watu ambao hawafahamu Kiingereza wala Kiswahili, kwa sababu tumekosa mwelekeo na fikra endelevi kuhusu wapi tunapoelekea? Ninawashukuru viongozi wa Tanzania kwa sababu wamewalazimu wale viongozi ambao wamejihusisha na ukombozi wa Afrika Kusini na Uganda, waliopitia Tanzania, kuzungumza Kiswahili. Juzi tulipokuwa katika uzinduzi wa Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki, tulikuwa na bahati kuketi kwenye meza moja wakati wa chakula cha mchana na Rais wa Afrika Kusini, Bw. Mbeki. Alikuwa anaongea Kiswahili, hata Wakenya wakaona aibu kwamba, yeye kwa miaka michache alipokuwa Tanzania wakati wa harakati za ukombozi wa nchi ya Afrika Kusini, alijifunza Kiswahili kilicho na msamiati muafaka, huku tukijigamba kwamba Kiswahili ni lugha yetu ya taifa, lakini tunazungumza vile watoto wetu wanavyozungumza, *Sheng*. Tunadhuru heshima ya lugha na ustaarabu.

Bw. Naibu Spika, nchi yetu ina shida kubwa sana hivi kwamba, kumeenea ukosefu wa adabu. Ustaarabu umeanza kudidimia kwa sababu hatuna mbinu za kuwaweka Wakenya pamoja ili wawe na utu unaowasawazisha. Yule anayeongea Kiingereza kizuri hajihusishi na mila za yule ambaye hajui Kiingereza. Kwa hivyo, ni vigumu kusawazisha uzalendo wetu. Matumizi na heshima kwa lugha zetu ndio msingi wa usawazishaji wa uzalendo wa Wakenya. Hili ni jukumu kubwa ambalo hatuwezi kuwaachia wanaofanya utafiti katika vitivo vya sayansi ya sanaa, ama katika vyuo vikuu peke yake. Ni jukumu letu kama viongozi wa kisiasa kuona kwamba tunaheshimu lugha zetu kuliko nyingine zote. Inafaa tuzingatia kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

Bw. Naibu Spika, kuna sehemu nyingi katika hili taifa letu ambako watu hawafahamu Kiingereza hata kidogo, kwa sababu historia haijawapatia fursa ya kuwa na mashule kama sehemu nyingine. Kwa hivyo, ni vigumu kuwasiliana na hao watu unapowatembelea. Ukiwa na mtalii anayezuru hapa nchini, inakubidi utafute mkalimani ili ufahamu mazingara yao. Unakuwa kama mtalii katika nchi yako. Haifai tuendelee kurudia kusema yale wengine wamekuwa wakisema kama kasuku bila kufikiria mbinu tunazofaa kutumia, ili kujikomboa kwa huu ufukara wa mawazo. Inafaa tutafute mbinu ambayo tutaitumia ili kuleta umoja miongoni mwa watu wetu, kutokana na kuheshimu mila zao na lugha zao, na haswa kuenea lugha ambayo hajihusishi na historia ya mkoloni. Tusipofanya hivyo, tutakuwa tumepoteza fursa kubwa.

Kwa hayo machache, ninaunga mkono Hoja hii.

The Minister of State, Office of the President (Mr. Sunkuli): Bw. Naibu Spika, ningependa kuunga mkono Hoja hii kwa kusema kwamba, taasisi hii ikiundwa, inafaa itilie mkazo lugha ya Kiswahili, kwa sababu, ingawa Kenya ina makabila mengi yanayozungumza lugha tofauti, itatubidi tutilie mkazo lugha ya Kiswahili. Wakati wakoloni walipofika hapa nchini, walikuta kwamba hatukuwa taifa kwa lolote, iwe ni lugha moja, mila na mambo mengi ya kushahibiana. Lakini, wakati Dr. Krapf alipofika Pwani ya Kenya, alijaribu kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuandika kamusi na vitabu vya Kiswahili.

Bw. Naibu Spika, mimi ningependa kutofautiana na wale ambao wamesema kwamba, kuna lugha moja ya Kiswahili. Hata wakati Dr. Krapf alipofika hapa Afrika Mashariki, alitambua kwamba, hata kule Pwani, hapakuwa na lugha ya Kiswahili moja. Kwa mfano, kuna kile Kiswahili kinachozungumzwa na mhe. Badawy; kuna Kiamu, na hata kile cha Mvita kinachozungumzwa na mhe. Nassir. Kwa hivyo, kuna lahaja nyingi za Kiswahili, kama vile Kiunguja, na kile ambacho kimeathiriwa na lugha zetu za kwanza. Ningependa kusema kwamba, hakuna namna moja ya kuzungumza Kiswahili ama hata Kiingereza. Kwa mfano, Waingereza wa Wales na wale wa England hawazungumzi kwa njia moja. Wazungu wa Amerika hawazungumzi kile "Kiingereza cha Malkia". Kwa hivyo, tusidharauliane kwa sababu pengine nitazungumza Kiswahili ambacho kimeathiriwa na lugha yangu ya Kimaasai. Hicho ni Kiswahili kwa sababu, kwa mfano, mhe. Muite atanielewa.

Bw. Naibu Spika, inafaa taasisi ya Kiswahili isawazishe lugha ya Kiswahili inayotahiniwa katika shule zetu. Inafaa tukuze Kiswahili ambacho kitaeleweka na kila mtu kama vile kilivyokuzwa na Dr. Krapf. Hatuwezi kuzungumza kama Watanzania. Na pia, kuna methali ambazo mtu anayetoka Pwani ataelewa, na yule wa kutoka Kilgoris asielewe. Kwa mfano, ukienda kule kwa Wamaasai na useme, kwa mafano: "Huyu hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini", hawatakuelewa. Watu wa Pwani wana mazingira tofauti na yale ya watu wabara. Kwa hivyo, hatuwezi kuzungumza Kiswahili kama Watanzania kwa sababu wana namna yao maalum ya kuzungumza Kiswahili.

Bw. Naibu Spika, kuna kwekwe ambayo "itakula" Kiswahili chetu, hasa watu wa bara. Kwekwe hii ni lugha

ya *Sheng*. Hii ni lugha ambayo imechangiwa na Kiingereza, Kiswahili na lugha nyingine. Watu wengi huizungumza hii lugha kama Kiswahili. Siku hizi, mimi sielewi Kiswahili kinachozungumzwa hapa Jijini. Kwa mfano, utasikia mtu akikuuliza: "Umeona *budaa* ama *mathee* wangu?" Au, "story zako ni deadly". Hiki si Kiswahili muafaka. Wengi wa watoto wetu wamezingatia lugha hii, na hatujui kama itamaliza ama kukuza Kiswahili. Kwa hivyo, inafaa hiyo taasisi ikiundwa, ijaribu kukomesha uundaji wa lugha inayoweza kumaliza lugha nyingine. Kiswahili ni lugha ambayo ina utamu wake. Hata mashairi ya Kiswahili ni matamu sana. Kuna kijana mmoja katika NYS kwa jina Ramadhan, ambaye akiimba mashairi ya Kiswahili, unatamani arudie. Kiswahili ni lugha yenye methali nzuri na ni lugha tamu, na itakuwa vibaya ikiwa itaharibiwa na *Sheng*. Bw. Naibu Spika, ningependa kumuunga mkono Mtumishi Kathangu kwa kuleta Hoja hii. Lakini siyo taasisi hii pekee yake ndiyo itakayokuza Kiswahili kama lugha ya taifa. Inafaa kila Mkenya aikuze lugha ya taifa. Kitambo kidogo, tulikuwa na stesheni moja ya radio, KBC, ambayo ilikuwa ikikuza lugha ya taifa, kwa sababu inatangaza kwa Kiswahili, na watu wanaweza kuelewa Kiswahili sanifu kupitia KBC. Lakini hivi sasa, kuna stesheni nyingine mpya ambazo hazikuzi lugha ya taifa. Kuna *Radio Kameme* ambayo inatangaza kwa Kikikuyu kitupu. Inafaa katika Bunge hili tukatae stesheni za redio za kikabila. Kwa sababu stesheni ambayo inaanzishwa kuzungumzia kabila moja haina faida. Mhe. Mbunge wa Kikuyu anasema ya kwamba Kikikuyu ni lugha ya taifa kwa sababu yeye anakubali kwamba Kabete ndio taifa la Kenya. Lakini akikubali kwamba Kikikuyu hakieleweki katika pande za Wilaya ya Trans Mara, basi hakitakuwa lugha ya taifa.

Nilipinga mimi mwenyewe mambo ambayo yaliandikwa na Bw. Ngugi wa Thiong'o kwamba waandishi wanaweza kuandika kitabu katika lugha yao peke yao na hali ni waandishi wa kitaifa. Hili si jambo la kukuza umoja na uzalendo wetu. Ni vizuri, kama tunataka kukuza lugha ya taifa, tuanzishe stesheni za redio za kitaifa, na waandishi wetu waandike kwa Kiingereza au Kiswahili kwa sababu hizo ndizo lugha ambazo zinaeleweka na kila mtu. Mhe. Badawy amesema kwamba Kiswahili kinachukuliwa kama somo la pili. Hata kwa magazeti, ni nani anayesoma gazeti la *Taifa Leo*? Watu wanaolisoma hili gazeti la *Taifa Leo* ni wale watu wa mashambani tu. Sisi wengine hapa, hakuna hata mmoja wetu ambaye ananunua gazeti la *Taifa Leo*. Labda rafiki yangu kutoka Kisauni alinunua kwa sababu kulikuwa na matangazo fulani ya kibiashara aliyotaka kutazama pale. Tunasema tu kwa kuongea kwamba tunataka kuunga mkono lugha ya kitaifa ya Kiswahili, lakini hatunui magazeti ambayo yameandikwa kwa Kiswahili. Inatubidi tutilie mkazo lugha ya Kiswahili na tusitumie lugha ya Kiswahili tu katika kuwazungumzia watu kutoka mashambani. Hata sisi wenyewe katika Bunge hili, ni vizuri tukuze hii lugha ili itumike kwa njia nyingi. Kwa hivyo, hata sheria za Kenya, inabidi zibadilishwe, zitafsiirwe na ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu watu wengi katika taifa hili wanaelewa Kiswahili wala si Kiingereza. Nimeona kwamba Mawaziri wenzangu, na hata wenzangu kutoka upande wa Upinzani, wanapotaka kusoma hotuba iliyoandikwa, hotuba zao haziandikwi kwa Kiswahili. Sijawahi kumwona mhe. Mbunge hata mmoja akisoma hotuba yake katika lugha ya Kiswahili. Kila mmoja anataka kusoma hotuba yake kwa lugha ya Kiingereza peke yake. Ni lazima tukisambaze Kiswahili ili kizungumzwe katika kila sehemu katika Kenya. Inafaa tusiogope kuzungumza Kiswahili chetu ambacho kimeathiriwa na lugha ya mama, bora kieleweke na msamiati uwe ni ule ule.

Mimi ninapenda vile watu wa Pwani wanavyozungumza Kiswahili. Wanakizungumza kwa maringo sana na inakuwa lugha nzuri, lakini mimi siwezi kuwaiga. Hiyo ni lugha yao waliyozaliwa nayo. Tukianzisha leo Kimaasai kuwa lugha ya taifa, hao watu wa Pwani watanitegemea mimi kwa jinsi lugha hii itakavyozungumzwa. Hii ni kwa sababu Kimaasai ni lugha yangu ya mama. Kwa hivyo, ningependa kuwasihii kwamba hata mkizungumza hapa, msioogope kuzungumza eti kwa sababu mtachekwa na rafiki yangu kutoka Kisauni kwa sababu yeye hajui lugha nyingine. Yeye anajua Kiswahili tu ambacho kinajaa mila za pale kwake.

Bw. Naibu Spika, ninaunga mkono.

Mr. Maitha: Bw. Naibu Spika, kwanza ningependa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niunge mkono Hoja hii.

Kabla sijatoa maada yangu ya leo, ningependa kumkosoa aliyeileta Hoja hii. Niliposimama kwa jambo la nidhamu, nilitaka kumrekebisha katika usemaji wake wa lugha kwa sababu unapoleta Hoja hasa, katika Bunge hili, ni lazima uwe umefanya utafiti. Kwa sababu ya umuhimu wa usemaji wa Kiswahili kama lugha, ni vizuri sana wakati tunapochangia na kutoa maada yetu katika Hoja kama hii, yaonekane kweli ni maada yanayohusiana na Hoja hii, na pia yawe na lengo la kukifanya Kiswahili kiwe lugha ambayo inazungumzwa katika hali ya ufasaha kabisa.

Mr. Deputy Speaker: Bw. Maitha, lengo la Hoja hii ni nini? Ni kuundwa kwa baraza la lugha za taifa.

Mr. Maitha: Bw. Naibu Spika, kwa kumkosoa aliyeileta Hoja hii kwanza, ningependa kutokubaliana na yeye kwamba ni baraza la kuunda lugha "za". Hii ni lazima iwe lugha "ya". Matamshi ya "za" na "ya" katika msamiati ni tofauti.

Mr. Deputy Speaker: Ni tofauti ndio, lakini hilo ndilo lengo lake. Kama unataka kuleta marekebisho, unakubaliwa kufanya hivyo.

Mr. Maitha: Ningependa kuendelea, Bw. Naibu Spika, kwa sababu nikimkosoa mhe. Mbunge aliyeileta Hoja hii, unamsaidia. Ningependa kwanza kabisa---

The Assistant Minister for Labour and Human resource Development (Mr. Maizs): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika. Mimi mwenyewe katika uamuzi na muundo wa lugha ya Kiswahili, ninaona kwamba msemu "lugha za taifa" ni sahihi kabisa. Tunaweza kusema "lugha moja ya taifa" lakini hatuwezi kusema "lugha nyingi ya taifa". Ni lazima tunyambue lugha kwa njia sahihi.

Mr. Maitha: Bw. Naibu Spika, ingawaje leo hatuko katika darasa, kama tungetaka kuwafundisha ndugu zetu ambao wangependa kusema Kiswahili safi, wangependa maana ya maneno "za" na "la". Lakini "za" na "la" katika msamiati, hayawezi kuwa tungo.

Nikiendelea katika maada yangu, ninamshukuru sana Mtumishi Kathangu ambaye aliileta Hoja ambayo inazungumzia kudumisha lugha ya Kiswahili. Kwanza ni lazima tuangalie na tuone uswahili ni nini. Kwa kweli, historia ya uswahili, hapo mwanzo, ulikuwa ukiitwa kingozi. Kingozi ni lugha ya watu wa Pwani wachache ambao waliishi kule Pwani na walikuwa wakizungumza Kingozi. Baadaye, Waarabu walipokuja, kwa Kiarabu mtu anayeishi Pwani huitwa "Msaal". Ukisema "Msaal", unamaanisha mtu ambaye anaishi Pwani na jina "Waswahili" lilitokana na neno "Msaal".

Lugha hii ilianza huko Pwani, na kwa sababu ni lugha ambayo inawajumuisha watu wote, ikawa ni lugha tamu na lazima idumishwe. Hata hivyo, ni makosa kusema kwamba ndugu zetu kutoka Tanzania ni Washahili. Ndugu zetu kutoka Tanzania wana Wamaasai, Wakikuyu na kila kabila, lakini kwa bidii yao, walikubaliana kuikuza lugha ya Kiswahili ili iwe ya wazalendo. Basi, mpaka sasa, wazalendo wote wa Tanzania huzungumzia lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa. Ndipo sasa sisi hapa katika Bunge hili tunaweza kukubaliana kuondoana utando wa macho. Kuondoa utando wa macho ni kusema kwamba tunaweza kuzungumzia lugha ya kigeni sana kwa sababu sisi ni wasomi, ama tunaweza kuzungumzia lugha ya Kizungu kushinda lugha ambayo tunaweza kuikuza sisi wenyewe kama wengineo. Unyevu wowote ambao hutanda nyasi ni ule ambao huja wakati wa usiku, lakini jua likitokea na likiangaza, unyevu ule huondoka.

Kwa hivyo, ni kama vile sisi tunavyozungumza Kiswahili hapa. Ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika Kenya unatakiwa utiwe maanani kwa sababu ni aibu kuona kiongozi, ama kuona mtu ambaye anastahili kupewa heshima yake kama kiongozi, akisimama mbele ya wananchi na kuzungumza lugha ya Kiswahili na kuichanganya na lugha ya kikwao. Pia, ni vizuri sana kutumia lugha ambayo inaeleweka na watu katika Kenya nzima kuliko kutumia lugha ambayo watu wengine hawaelewi.

Bw. Naibu Spika, hivi majuzi, katika Mkoa wa Pwani, niliona Waziri anayehusika na utamaduni na mambo ya akina mama akiwahutubia wananchi wakati wa kusherehekea siku ya wanawake duniani. Aliwasomea wanawake wengi ambao hawakuelewa lugha ya Kiingereza, hotuba ya ulimwengu mzima kwa lugha hiyo. Ile hotuba ingetafsiriwa kwa Kiswahili. Ilikuwa inasomewa katika uwanja wa Manispaa ya Mombasa, na akina mama wengi waliokuwepo walikuwa Waswahili. Hii ni aibu moja ya Mawaziri wetu. Wamechukulia lugha ya Kiingereza huzungumzwa kila pahali, hata mbele ya Wazungu.

Katika kujua Kiswahili, rafiki anayetoka Umaasaini amezungumza mengi. Hiyo ni kuonyesha kwamba, yeye ana riwaya ya uswahili. Ana habari kuhusu Kiswahili. Uswahili mwingi unaozungumzwa kule Pwani umechanganyika. Kuna Uswahili wa riwaya, tamthilia na kadhalika. Lakini lengo kubwa ni kwamba, wakati tutakapoliunda baraza hilo, ni lazima liwe na ukamavu wa usemaji wa lugha. Wenye lugha mara nyingi huwa ndio wenye lugha. Wanapoisema, huja na utamu wake. Kwa hivyo, baraza hilo likiwa linaweza kushirikiana na taasisi mbali mbali, hasa Wizara ya Elimu--- Ngingependa kuilaumu Wizara ya Elimu kwa kitu kimoja. Usemaji na usomaji wa Kiswahili katika shule zetu unachukuliwa kwa mzaha. Watoto wetu wakizoeshwa lugha wakiwa shuleni, ziwe za msingi, upili na vyaoni, Kiswahili Kenya kitakuwa kinazungumzwa bila matatizo yoyote. Lakini utakuta mashule mengine yanawakataza wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili. Utakuta ya kwamba hata adhabu hutolewa kwa wale wanafunzi wanaopatikana wakizungumza Kiswahili.

Ikiwa Bunge hili litapitisha Hoja hii leo, lazima kuwe na njia za kuhamasisha wanaotaka kuzungumza lugha ya Kiswahili. Lazima wapewe nafasi ili waizungumze lugha hiyo vile wanavyotaka. Sisi tunaopenda kuzungumza lugha hiyo, ni tamu sana. Mara nyingi, katika Bunge hili, mhe Kathangu amejaribu kutumia lugha ya Kiswahili kila wakati. Hata sisi wenyewe tunaotoka sehemu ya Pwani mara nyingi tunajaribu kuikwepa lugha ya Kiswahili, ili tuzungumze lugha za kigeni. Lakini, hata hivyo, dau likipiga mwamba, ni lazima omo liumie! Hapo tunasema ya kwamba, mwamba ukipigwa, hauonekani. Tutaendelea kuunga mhe. Kathangu mkono kwa sababu lugha ya Kiswahili ina utamu wake.

Bw. Naibu Spika, nikimalizia, nataka kusema kwamba, Wizara inayohusika na kuleta makadirio ya pesa katika Bunge hili, ifanye hivyo kwa lugha ya Kiswahili. Makadirio yanapaswa kujulikana na kila mtu, awe mdogo au mkubwa. Hata pesa tunazotumia zinaandikwa kwa Kizungu kama pauni au dola. Watu hawajui aina hizo za pesa. Kama tungeandika makadirio kwa lugha ya Kiswahili, watu wengi wangepelekewa stakabadhi hizo ili wazisome. Watajua sisi tumeikabidhi Serikali pesa ngapi ili wazitumie.

Kwa hayo machache, naunga mkono.

Mr. Kombe: Bw. Naibu Spika, nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kumuunga mkono Mtumishi Kathangu kwa kuleta Hoja hii ya muhimu. Hoja hii inalitaka Bunge hili kupendekeza kuundwa kwa baraza la lugha za taifa, ambalo litafanya kazi na Wizara mbali mbali zinazohusika, ili kujenga uzalendo, utamaduni, fasihi na utambuzi wa kitaifa kupitia lugha zetu.

Bw. Naibu Spika, naunga mkono Hoja hii kwa sababu chache zifuatazo. Kwanza, ni kuhusu vile ambavyo tumetekwa, au tumechukuliwa mateka na Waingereza. Mwingereza alipokuja hapa nchini, alitulazimisha kufanya mambo yake aliyokuwa anayaelewa. Alitulazimisha kuzungumza lugha yake kutoka ng'ambo. Tumewekwa chini ya ukoloni miaka mingi. Natambua ya kwamba, tulipoanza kupigania Uhuru, tulisema tunataka kujitegemea, tuwe huru na tuweze kufanya mambo ambayo yanahusu utamaduni na uzalendo wetu. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba, baada ya kupata Uhuru, tuliendelea kukaa na tabia na ustaarabu wa Kiingereza. Tuliendelea kuzungumza lugha ya Kiingereza ambayo ni ya kigeni. Baada ya kutoka kwenye ukoloni, bado tuko katika hali ya umateka. Nasema hivyo kwa sababu nilipokuwa nikisoma katika shule ya msingi, walimu wetu wa Kiingereza walitulazimisha kuzungumza lugha ya Kiingereza. Tulisahau kuzungumza lugha zetu muhimu za nchini. Wakati huo, ukizungumza lugha nyingine, ulikuwa unapewa adhabu ya kuvishwa gogo zito na kutandikwa viboko vingi kwa sababu ya kuzungumza lugha yako au Kiswahili. Hiyo inadhihirisha kwamba, bado tuko chini ya ukoloni. Mpaka sasa, unapotembelea nyumba za marafiki katika nchi yetu, au mitaa tunayoishi, utawasikia watoto wetu hawazungumzi lugha nyingine, ila ni Kiingereza. Na hiyo haitatimarisha katika utamaduni na kizalendo. Kwa hivyo, ninaunga mkono kabisa kwa moyo wangu wote kwamba Baraza hili la Lugha za Taifa liweze kuundwa ili liimarisha lugha zetu za hapa nchini.

Bw. Naibu Spika, nilipoingia hapa Nairobi miaka mingi iliyopita, kama 30 hivi, nilikuwa najua Kiingereza kidogo na Kiswahili kidogo. Nilipofika hapa Nairobi nikasikia lugha nyingine geni ambayo ilikuwa ikisemekana kuwa ni Sheng; na nikapitia mtaa mmoja na nikasikia mtoto mdogo akizungumza na mwenzake kwamba alikuwa amekasirishwa na alipokasirishwa, nikamsikia akisema maneno haya: "Nikakipiki kiotoni nikamgei nacho". Sasa sikuelewa hii ni lugha gani. Si Kiingereza, Kikikuyu, Kijaluo na wala si Kiswahili. Nilipouliza wenzangu, nikaambiwa kwamba yule kijana alikuwa anamaanisha kwamba aliokota jiwe na akampiga nalo. Sasa, uchanganyikaji wa maneno ya lugha mbali mbali hauwezi kuimarisha utamaduni na uzalendo wetu. Ningesema hivi: Baraza hili laweza kuundwa haraka, liweze kusimamia na kuimarisha lugha zetu za kitaifa hasa lugha hizi za makabila makubwa kama Kikikuyu, Kijaluo ama Kigiriyama, ili siku nyingine tunapoiningia hapa Bunge, Wamaasai, Wajaluo na Wakikuyu waweze kusema lugha zao ambazo pia wengine watakuwa wanazielewa. Hiyo nafikiri itatuimarisha katika mawasiliano yetu ya kitaifa.

Bw. Naibu Spika, hapa tuna ugumu. Kuna wengine katika Bunge hili hawaelewi vizuri Kiingereza. Kuna wengine pia hawaelewi Kiswahili - itakuwa ni jambo la busara Bunge hili, siku za mbeleni, ikiwa lugha za taifa zitakuwa zimeimarika, kila mtu aruhusiwe kuzungumza ile lugha ambayo anaelewa na ambayo inaeleweka na wale wengine. Baraza hili litakuwa lina kazi ya kufundisha na kuimarisha zile lugha nyingine, ili mawasiliano nchini yaweze kuwa rahisi. Mjaluo anapotoka kule Siaya akifika Mombasa, hajui Kiswahili na akiwa anajua Kiingereza na Kijaluo peke yake, hawezi kufanya mawasiliano na hiyo inataabisha na inaleta ugumu katika hali ya kuelewana. Sisi wananchi wa Kenya wenyewe tumechukuliwa mateka na lugha ya kigeni ambayo ni Kiingereza.

Bw. Naibu Spika, wacha nikupatie mfano. Nilipoenda kusoma kule Uingereza miaka mingi iliyopita, nilipata Mzungu mmoja aliyekuwa amepitia katika nchi zetu za Afrika Mashariki, na aliposikia kwamba kuna Mkenya hapa anayesoma katika chuo kikuu fulani, akaja na akawa anatamani kuongea lugha ya Kiswahili. Jambo la aibu ni kwamba sikujua Kiswahili kingi zaidi ya yule mgeni aliyekuwa hapa. Nakwambia kama Baraza la Lugha za Taifa lingekuwa hapo awali, mimi singeaibika kule Uingereza kung'ang'ana na kuzungumza lugha ambayo inasemekana kwamba ndio yetu. Ni jambo la aibu.

Bw. Naibu Spika, unapofika Ufaransa siku ya leo, utajaribu kuzungumza Kiingereza na Mfaransa lakini atakujibu kwa Kifaransa. Kwa sababu gani? Yeye anasikia kwamba ni vizuri kuzungumza lugha yake. Hapa Kenya, mgeni anapokuja, Mkenya atakuwa ni wa kwanza kuzungumza lugha ya kigeni kwa sababu yeye haoni maana ya kuzungumza zile lugha ambazo zinaimarisha utamaduni wa nchi ya Kenya. Kuna umuhimu wa sisi wazalendo wa nchi ya Kenya kujua lugha hizi muhimu, na kuweza kuwasiliana na wenzetu wa hapa nchini katika hali ya uzuri na wema.

Mr. Maitha: Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Kufikia hapo tungetaka Kiti chako kitupe mwongozo. Tunazungumza juu ya Kiswahili, na Hoja hii imeandikwa: "Baraza la Lugha za Taifa". Sasa ningetaka Kiti chako kituambie kama tunazungumzia juu ya Kiswahili ama hata lugha za Kigiriyama na Kijaluo tuwe tunaweza kuzungumza?

The Assistant Minister for Labour and Human Resource Development (Mr. Maizis): Jambo la kufahamisha, Bw. Naibu Spika. Mheshimiwa huyo haelewi lengo la Hoja hii. Ni lugha zote za Kenya wala si Kiswahili pekee.

Mr. Deputy Speaker: Hoja hii inauliza sisi Wabunge kufanya nini? Inatuuliza kukubali kwamba Baraza la Lugha za Taifa libuniwe, na hakuna taabu kuwa na zaidi ya lugha moja au mbili za taifa. Kule Afrika Kusini Wabunge wanatumia lugha 11 na zinatafsiriwa. Kila Mbunge anaposimama kusema kwa lugha yake, inatafsiriwa wakati huo huo

kwa lugha ya wale Wabunge wengine. Kwa hivyo, hakuna taabu yoyote kuwa na lugha zaidi ya moja ya kitaifa. Endelea!

Mr. Kombe: Bw. Naibu Spika, inakasirisha kuona kwamba sisi Wakenya wenyewe tumedharau lugha zetu maanake---

Naunga mkono.

Mr. Maore: Bw. Naibu Spika, natoa shukrani pia kwa kutunikiwa nafasi niongee juu ya Mswada huu. Pia nami ningetaka kutoa maoni kwamba kuwe na Baraza la Lugha za Taifa ambalo litafanya kazi ya Wizara mbali mbali zinazohusika, ili kujenga uzalendo, utamaduni, fasihi na utambuzi wa kitaifa kupitia lugha zetu.

Bw. Naibu Spika, mpaka mhe. Kombe alipoanza kuongea, wale wengi walioongea hapo awali wameongea kama ni lugha ya Kiswahili tunayozungumzia. Nakubali kwamba nchi ikiwa ya mchanganyiko kama hii yetu, ni vizuri tuweze kuwa na baraza litakaloweza kuhifadhi zile mila, tamaduni na lugha tofauti tofauti ambazo zinaweza kuunda taifa la Kenya. Ukiangalia katika vyyo vingi vikuu huko Marekani, utakuta kuna mafunzo ya lugha za Kigiriki, Kiitaliano, Kihispania, Kiingereza, Kijerumani, Kijapani na hata Kituruki. Utakumbuka yule mtu aliyeuzwa kutoka hapa anayeitwa Ocalan, ambaye alipatiwa serikali ya Uturuki; ile hatia kubwa amewahi kufanya ni kwamba watu karibu 7 milioni hawaruhusiwi kuongea lugha yao. Kwa hivyo, kumnyima mtu fursa ya kuongea lugha yake pia inaweza kuwa ni hatua ya kikoloni. Wakoloni walipokuja na wakatoa amri katika Wizara ya Elimu kwamba watu wasiwe wanaongea lugha za mama kwa sababu ni za kishenzi, tulivuta hiyo kasumba. Mpaka leo, utakuta ni hatia mara nyingi kwa watu kuongea lugha za mama katika shule zetu.

Bw. Naibu Spika, ningependa kutoa shukrani kwa mwaanzilishi wa taifa la Tanzania, ambaye alianza kwa kuandika kamusi na akaandika vitabu vingine katika lugha ya Kiswahili. Tuna mashujaa kama vile Ibrahim Hussein na Shabaan Roberts ambao wamewahi kutoa mchango mwingi kwa lugha ya Kiswahili. Lakini hapa - ulimsikia Waziri katika Ofisi wa Rais alipokuwa analalamika juu ya Bw. James Ngugi hapo awali kabla hajabadilisha kuitwa Ngugi wa Thiong'o - ni vizuri watu kuenda na waandike vitabu kwa lugha zile wanaelewa zaidi.

Bw. Naibu Spika, wengi wetu ambao tumewahi kusoma katika shule kwa muda wa zaidi ya miaka saba na tunaendelea zaidi na zaidi, shida ni kwamba unafikiri katika lugha ya mama halafu unatoa mawazo yako kwa lugha ya pili, kama Kiingereza. Hii ndio sababu tunasema kwamba, katika nchi hii ya Kenya, yafaa tuwe na Baraza la Lugha za Taifa, ili iwe hatua ya kwanza kuonyesha kwamba tuna mwelekeo wa kitamaduni na kizalendo. Hata tukisema kwamba Lugha ya Kiswahili iwe lugha ya taifa, tuwe na baraza hili ambalo linaweza kuhifadhi, kutunza na kufanya uchambuzi mwingi kwa zile lugha nyingine ambazo ni zaidi ya 40.

Bw. Naibu Spika, katika kuyachambua maneno ya filozofia, sayansi, na lugha nyingine nyingi, pamoja na hesabu, ni vizuri tuweze kupata nafasi ya kuhifadhi lugha nyingi ambazo zilikuwa na utajiri wa maneno na mambo mengi. Yapata miaka 21 au 22 iliyopita, kulikuwa na ule mwito wa kuanzisha Elimu ya Ngumbaru; elimu ya watu wazima. Ilifika wakati fulani ambapo Serikali ilisahau ule mwongozo wake. Watu wengi ambao wangufaika kutokana na huo mradi wa Serikali, hadi leo, hawajafaidika, na hatujui ni kwa nini Serikali haikutilia mkazo na kuhakikisha kwamba kila mwananchi anajua kusoma na kuandika. Kama vile tunavyojua, Serikali hii imekuwa na mambo mengi; inaanzisha mradi asubuhi, saa sita inaanzisha mradi mwingine, na jioni inaanzisha mwingine bila kufuatilia ni mradi gani itakaotekeleza kwanza.

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika. Mbunge mwenzangu amesema kwamba, Serikali hii inaanzisha mradi fulani asubuhi; saa sita inaanzisha mradi mwingine, na saa za joini mradi mwingine. Sijui anaeleza kuhusu Serikali gani! Anaweza kutufanulia na kutueleza ni miradi gani ambayo tumeanzisha leo asubuhi na kufika saa sita mchana tukaanzisha mradi mwingine, na jioni tukaanzisha mradi mwingine?

Mr. Maore: Bw. Naibu Spika, sijui kama tunaishi katika sayari moja na Waziri.

Dr. Kituyi: Jambo la ufahamisho, Bw. Naibu Spika.

Mr. Deputy Speaker: Order! Disallowed!

Mr. Maore: Nalikubali, Bw. Naibu Spika.

Dr. Kituyi: A point of information is allowed, Mr. Deputy Speaker, Sir!

Mr. Deputy Speaker: Hakuna kitu kama hicho!

An hon. Member: Ni kitu gani hicho!

Mr. Maore: Bw. Naibu Spika, Waziri anaonekana kama anatoka sayari nyingine. Hajui kwamba Serikali hii, katika mwaka wa 1978, ilianzisha mradi wa maziwa kwa watoto wa shule. Leo hii, yeye hawezi kueleza maziwa hayo yalienda wapi. Mwaka huo huo, Serikali ilianzisha mpango wa elimu ya ngumbaru; leo Waziri hawezi kueleza mradi huo uko wapi. Katikati mwa mwaka wa 1991, walianzisha mradi---

An hon. Member: Walianzisha mradi wa lugha gani?

Mr. Maore: Bw. Naibu Spika, ninamjibu Waziri kuhusu miradi ambayo nasema Serikali ilianzisha na

haijawahi kutekeleza.

Bw. Naibu Spika, katikati ya mwaka wa 1980, Serikali ilianzisha mfumo wa elimu wa 8-4-4. Jambo hili limeliangusha taifa zima. Miaka hiyo hiyo, walianzisha mradi wa District Focus for Rural Development; Waziri hawezi kueleza huyu ni "mnyama" gani. Hii ndio sababu nilikuwa nasema kwa heshima, bila kuingilia hayo maneno, kwamba, Serikali hii haina mbele wala nyuma!

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika. Umesikia vile Mbunge huyo amefafanua hapa. Ametaja miaka; 1978 na 1984, lakini hiyo sio asubuhi; hiyo ni miaka! Kusema kweli, hiyo miradi yote ambayo Mbunge huyo amegusia tumeitekeleza na imefaulu.

Mr. Deputy Speaker: No, no! Mheshimiwa Maore alikuwa anatoa mfano tu. Kwa hivyo, sidhani alikuwa anasema kuwa unaamka asubuhi na kuanzisha miradi---

The Minister for Medical Services (Dr. Anangwe): Alisema hivyo!

Mr. Deputy Speaker: La, lakini nilimwelewa kwamba alikuwa anatoa mfano. Endelea!

Mr. Maore: Bw. Naibu Spika, natoa shukrani kwako kwa huo ufafanuzi. Hii ndio sababu tunasema kwamba, yafaa tuwe na baraza la kitaifa. Kwa mfano, kuna wamishenari wanaokuja hapa nchini na kuelekea upande wa Turkana, Maasai na wengine wanaenda huko Meru, Ukambani na hata kwa Waborana. Wakija hapa na kupiga simu mahali fulani, wataambiwa, "Mahali unapokwenda, ni vizuri ujitayarishe kwa miezi miwili, mitatu, minne hadi mitano, ukijifunza lugha ya huko." Ukitaka kujifunza lugha sanifu ya Kimeru, unaketi na kupatiwa zile kamusi na Biblia ambazo zimeandikwa kwa hiyo lugha na kufundishwa na mtu ambaye anajua lugha ambayo ni sanifu katika sehemu unayokwenda.

Ukitaka kujua ni mila gani utakazohitaji kuelewa kabla hujaanza kufanya kazi, unaelezwa. Hii ndio sababu tunasema kwamba, nchi kama ya Kenya itanufaika zaidi tukiwa na baraza ambalo linaweza kuunda taasisi maalum za uchunguzi wa lugha na mila mbali mbali, ili ziweze kuhifadhiwa kuwa za manufaa kwa vizazi vijavyo. Shida zilizoko katika kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili ama lugha nyingine za kitaifa ni kwamba, kuna hitilafu katika upeo. Ukishapata hati ya lugha, kwa mfano, lugha ya Kiswahili ama lugha nyingine yoyote ile, uende upate shahada katika chuo kikuu. Mara nyingi kumekuwa na manufaa kwa wale wanaojifunza lugha za Kifaransa, Kijerumani, Kiingereza na Kihispania. Wakienda katika chuo kikuu, wanapata usaidizi kutoka kwa hizo serikali tofauti tofauti wanakoenda. Hii ndio sababu Hoja hii inahimiza watu wengi kujifunza lugha hizo badala ya lugha zile nyingine za taifa.

Bw. Naibu Spika, naunga mkono Hoja hii ili tuwe na Baraza la Lugha za Taifa la kuweza kusimamia lugha zetu.

Mr. Deputy Speaker: Tuna masaa mawili ya kujadili Hoja hii. Sasa zimebaki dakika 30 tu. Kwa hivyo, sasa nitamuomba mwakilishi wa Serikali ajibu.

[Mr. Deputy Speaker left the Chair]

*[The Temporary Deputy Speaker
(Mr. Poghiso) took the Chair]*

The Assistant Minister for Education, Science and Technology (Mr. Karauri): Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I will support this Motion because in the last sentence, it reads: "Bunge hili linapendekeza uundaji wa Baraza la Lugha za Taifa." This is because it should not be misunderstood to mean other languages which are not national languages because the Motion reads, "lugha za taifa"; national languages.

Mr. Deputy Speaker, Sir, I want to inform the Mover of the Motion that, already, we have a National Council for Kiswahili. The Mover has also recognised that Kiswahili Language is taught in all our schools and, in fact, it is an examinable language. The best way to propagate a language is to teach it. The Government has ensured that Kiswahili is taught in schools, so is English.

In fact, in this country, our national language is Kiswahili, and English is our official language. So, we are taking care of those two languages. But if we were to enhance or promote tribal languages, we would not be creating harmony; rather, we would be creating disharmony.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, the Mover of this Motion has said that there are 59 languages in this country. If we were to promote all of them, we would create more confusion than harmony in this country. However, we intend to continue promoting the national and the official languages spoken in this country. At the same time, I wish to urge Kenyans and Members of Parliament in particular to read. There is no language that grows without people using it either by speaking or reading it. I know that Members of Parliament here do not read a lot. In fact, some of us have even difficulties reading all the materials that come to this House, including Bills and Motions. So, everybody in this country, including Members of Parliament should be encouraged to read more and more materials in Kiswahili and English so that the language grows. By so doing, they will know how to speak it and express themselves.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I do not want to spend a lot of time on this Motion because we are supporting it as a Government. In fact, what it is asking for is already in place. So, we have no reason to reject it.

With those remarks, I beg to support.

Mr. Raila: Asante sana, Bw. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Hoja hii ambayo ni muhimu kwa taifa letu.

Bw. Naibu Spika wa Muda, Waswahili husema; "Mwacha mila ni mtumwa." Msingi muhimu wa mila ni lugha. Taifa ambalo haliheshimu lugha zake ni taifa ambalo limekashifu mila. Inafaa sisi Wakenya tukubali kwamba taifa la Kenya lina makabila 42 na kila kabila lina lugha yake. Hizo lugha 42 ni muhimu. Hakuna moja ya hizo lugha ambayo ni muhimu kushinda nyingine. Lakini miaka 37 baada ya kupata Uhuru, bado tunayaendesha mambo yetu tukijidanganya kwamba lugha muhimu ni Kiswahili na Kiingereza peke zake. Huu ni upotovu! Yafaa tufanye marekebisha ili tuweze kutambua na kuheshimu lugha nyingine za makabila yetu. Kule Afrika Kusini, wametambua lugha 11 kama lugha za taifa. Mwaka jana, nilikuwa katika Bunge la Afrika Kusini, kule Cape Town, na nilistaajabu kuona kwamba kuna vifaa vya kutafsiri lugha. Kama mhe. Mbunge anachangia Hoja fulani, Wabunge wengine wanaweza kuchagua ile lugha ambayo wanapenda kusikiza kama vile, Kikaburu, Kizulu, Kishona, Kisuthu, Kixhosa au lugha yoyote ile kati ya hizo 11. Kwa hivyo, watu wako huru kutumia lugha wanayoipenda. Ni kweli kwamba siyo kila mmoja wetu hapa anaweza kuongea vizuri kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Wakati mwingine mhe. Mbunge anaweza kuwa anataka kuongea juu ya Mswada au Hoja fulani lakini utapata kwamba kwa sababu ya viziuzi ambavyo tumewekewa, inakuwa vigumu kufanya hivyo.

Bw. Naibu Spika wa Muda, ya muhimu zaidi ni kule katika baraza za wilaya. Kwa nini baraza za wilaya zinaitwa local authorities kama watu wanazuiliwa kuongea lugha za kikwao? Kwa nini mtu analazimika kule Nyeri County Council kuongea kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili na hali anaongea na Wakikuyu wenzake? Kama mtu haelewi Kikuyu, ni kwa nini anapelekwa kufanya kazi miongoni mwa Wakikuyu? Hiyo ndiyo maana ya local authority. Watu wa sehemu hiyo wafanye kazi katika local authority hiyo. Wakitaka kuongea lugha ya taifa, waajiriwe katika Wizara za Serikali. Ni kwa nini baraza za wilaya kule Meru inaendesha mambo yake kwa Kiingereza? Mtu anayechaguliwa katika baraza ya wilaya ni mtu mwenye elimu. Elimu haimaanishi kwamba unaweza tu kuongea Kiswahili na Kiingereza! Ni mtu ambaye amelimika na ni mzee ambaye ana ujuzi wa kutosha lakini utapata kwamba anazuiwa kuongea pale sawasawa kwa sababu akijaribu kuongea Kiswahili au Kiingereza, hawezi. Ni kwa nini Wasomali kule Wajir wanalazimishwa kuongea Kiswahili? Kitu muhimu siyo lugha ambayo mtu anatumia bali ni maneno anayotoa.

Bw. Naibu Spika wa Muda, ni lazima tufanye utafiti katika lugha za kiasili ili tuweze kuzitajirisha. Kwa mfano, tuna kamusi ya Kijaluo ya Kibiolojia. Pia wameandika nyingine ya Kibotania. Hayo ni matokeo ya utafiti wa muda mrefu ambao umefanywa na Prof. Kokwaro. Hiyo itawasaidia watoto wa Wajaluo ambao wamezaliwa Nairobi, Mombasa na kila mahali kujua majina ya miti kwa lugha ya Kijaluo. Hiyo ndiyo njia ambayo tunaweza kuyaimarisha maendeleo katika nchi yetu. Ni lazima tuzitambue lugha hizi zote. Kule Ujerumani, kuna kabila ndogo linalojulikana kama Slovenia. Hawa watu wametambuliwa kama Waslovenia na lugha yao inafundishwa katika shule na wanaongea lugha yao katika baraza za wilaya. Hivyo ni kulinda haki za walio wachache.

Bw. Naibu Spika wa Muda, tuunde baraza la kitaifa ambalo litaimarisha hali ya utafiti katika lugha za kijadi ili watu wetu waweze kuongea na kujivunia lugha zao. Hii ndiyo tunaita kwa Kiingereza "unity in diversity".

Bw. Naibu Spika wa Muda, sisi kama taifa ni lazima tujiivunie lugha yetu. Ukienda huko Marekani, utaona kama hawana raha kwa sababu wanatumia lugha moja tu. Lakini hapa kwetu, wakati ninaposikia Wameru, Wakamba, Waluhya au Wasomalia, wakiongea upande ule ninajivunia kuwa Mkenya, kwa maana ninaona huo ndio utajiri wa nchi yetu ya Kenya. Hiyo ndiyo sababu Rais wa kwanza wa nchi hii, Mzee Kenyatta, alijaribu sana kuendeleza lugha yetu ya kitaifa ya Kiswahili kila mahali alipokuwa anakwenda na hata hapa, alikuwa amehimiza matumizi ya Kiswahili.

